

Wanawake wa CCM Mkoa wa Dar es Salaam wakicheza kwenye mkutano wa kampeni za uchaguzi za CCM zilizofanyika kwenye viwanja vya Leaders Kinondoni jijini Dar es Salaam jana.**Picha na CCM**

# Samia atangaza mageuzi mapya usafirishaji Dar

> **"Nataka niwaamble maandamano yatakayokuwapo ni watu kwenda vituoni kupiga kura, hakuna maandamano mengine yatakuwapo, hakuna tishio la kiusalama litakalokuwapo, anayesema ni Amiri Jeshi Mkuu wa nchi."**
> Samia Suluhu Hassan

**Janeth Mushi,** Mwananchi
jmushi@mwananchi.co.tz

Dar es Salaam. Mgombea urais wa Tanzania kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM), Samia Suluhu Hassan ameahidi kukamilisha miradi mikubwa itakayoongeza kasi ya biashara na kukuza uchumi wa Jiji la Dar es Salaam, iwapo atachaguliwa kuendelea kuongoza nchi kwa kipindi kijacho.

Akizungumza jana katika mkutano wa kampeni uliofanyika kwenye Viwanja vya Leaders Club, Samia alisema Serikali yake itaendelea kuboresha miundombinu ya jiji hilo kwa kujenga madaraja ya juu (flyovers), mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) na kuboresha barabara kuu zenye msongamano mkubwa.

Alieleza kuwa miradi itakayotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa daraja la juu kutoka Morocco–Mwenge hadi Magomeni, pamoja na uboreshaji wa barabara za Ali Hassan Mwinyi na Umoja wa Mataifa, ili kupunguza msongamano wa magari na kuongeza ufanisi katika shughuli za biashara.

**Mradi wa BRT**

Samia alisema sekta binafsi imeanza kutoa huduma za usafiri kupitia mradi wa BRT, ambao ujenzi wake umefikia asilimia 61 na tayari kilomita 94.9 za barabara zimekamilika, huku Sh2.1 trilioni zikiwa zimetumika.

Aliahidi akipata ridhaa ya wananchi, Serikali yake itahakikisha awamu zote za mradi huo zinakamilika na kuendeshwa kwa ufanisi na sekta binafsi.

"Sekta binafsi wataendesha mabasi hayo kwa kupakia abiria. Kampuni ya ENG imeingiza mabasi 177, YG Link mabasi 166, Metro City mabasi 334 na Mofat mabasi 255 ambayo yako njiani. Kuanzia Januari 2026 mtaona mageuzi makubwa katika huduma za mabasi ya mwendokasi," alisema.

Aliongeza kuwa mradi huo unaipa Tanzania sifa kimataifa kwa ubora wa uwekezaji wake na utakuwa chachu ya mageuzi makubwa katika usafiri wa jiji hilo.

**Miundombinu ya barabara**

Kuhusu uboreshaji wa barabara, mgombea urais huyo alisema anatambua changamoto za uchakavu na uharibifu wa miundombinu kutokana na mvua kubwa zilizonyesha kwa nyakati tofauti na kwamba, Serikali itakamilisha barabara zote zilizoko katika hatua za ujenzi.

Amezitaja baadhi ya barabara hizo kuwa ni Kimara–Mavurunza–Bunyokwa–Kinyerezi yenye urefu wa kilomita saba, inayopita katika majimbo ya Segerea, Kibamba na Ubungo.

Alisema pia Serikali itaongeza bajeti kwa ajili ya barabara mpya zitakazokuza maendeleo ya jiji hilo.

"Tutapanua barabara ya Mwai Kibaki (Morocco-Kawe) yenye urefu wa kilomita tisa na barabara ya Tegeta-Bagamoyo yenye urefu wa kilomita 57," alisema Samia.

Kwa Jimbo la Ubungo, mgombea huyo ameahidi kukamilisha barabara ya Kibamba-Mloganzila yenye urefu wa kilomita nane, sambamba na kuboresha barabara za ndani.

Akizungumzia mafuriko, Samia alisema Serikali yake itatatua tatizo la mafuriko katika maeneo yanayopakana na Mto Gide, Mto Mbezi na Mto China kupitia awamu ya Pili ya Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam (DMDP), pamoja na kuboresha mifereji ya maji katika maeneo ya Magomeni, Tandale na Makumbusho.

Kwa upande wa usafiri wa daladala, Samia alisema Serikali itakamilisha ukarabati wa stendi za Mwenge, Kawe, Bunju B na Tegeta Nyuki, ili ziwe na miundombinu bora na mpangilio wa safari.

**Miradi ya maji**

Mgombea urais Samia ameahidi kuendelea kutekeleza miradi mikubwa ya maji itakayohudumia mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro, ikiwamo mradi wa kutoa maji kutoka Mto Rufiji unaolenga kumaliza tatizo la maji hasa wakati wa kiangazi.

Aidha, alisema Serikali itaharakisha kukamilika kwa bwawa la Kidunda lenye thamani ya Sh336 bilioni litakalosaidia kuongeza upatikanaji wa maji safi na salama.

"Mradi wa Rufiji tumeanza kwa upembuzi yakinifu na utafiti wa kina. Awamu hii tutaanza utekelezaji ili Dar es Salaam ipate maji ya uhakika kutoka Kidunda, Ruvu na Rufiji," alisema.

Mkoa wa Dar es Salaam nao unakabiliwa na migogoro ya ardhi, hivyo, Samia ameahidi kufanyia kazi kero hiyo akipatiwa ridhaa Jumatano Oktoba 29, 2025.

Alisema migogoro hiyo imekuwa changamoto kubwa, kwa sababu kiwanja kimoja huuzwa kwa watu hadi zaidi ya wanne, hususan katika maeneo ya Mabwepande, Mbweni, Bunju, Madale na Nyakasangwe.

Alisema Serikali inaendelea na juhudi za kuratibu, kurasimisha na kutatua migogoro hiyo kupitia ofisi za mkoa na wilaya.

Alisema Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) limeanza kuwekeza kwenye ujenzi wa nyumba za viwango tofauti jijini humo na Serikali ya CCM itatekeleza mpango maalumu wa 'Mama Samia Housing' utakaolenga kupunguza uhaba wa makazi bora kwa wananchi.

**Aonya maandamano**

Akizungumzia hoja za maandamano, Samia ambaye ni Rais wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, alisema maandamano yatakayofanyika Oktoba 29, 2025 ni ya kwenda kwenye vituo vya kupiga kura, huku akiwataka Watanzania kumwachia matusi kwa kuwa anayabeba kwa niaba yao.

Alisema Watanzania wawe na amani kwa kuwa hakuna tishio la kiusalama litakalotokea siku ya uchaguzi mkuu na amewaomba wakichague Chama cha Mapinduzi.

"Niwahakikishie kuwa Oktoba 29, 2025 keshokutwa, tokeni mwende mkapige kura, ninayeongea hapa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa nchi hii. Nataka niwaambie maandamano yatakayokuwapo ni watu kwenda vituoni kupiga kura, hakuna maandamano mengine yatakuwapo, hakuna tishio la kiusalama litakalokuwapo, anayesema ni Amiri Jeshi Mkuu wa nchi," alisema.

Ameongeza: "Niwaombe ndugu zangu twendeni tukapige kura, baba ukitoka hakikisha unatoka na familia nzima kila aliyeandikishwa. Mabalozi wetu tokeni na watu wenu wote mkapige kura, twendeni mkaheshimishe CCM, tukaiheshimishe Tanzania tukapige kura kwa usalama turudi kwa usalama."

Alisema aliapa kutumikia Tanzania na ndicho anachokifanya, aliapa kulinda nchi, kujenga utu wa Mtanzania na kuheshimisha na kuwa anapohakikisha watu wanapata majisafi, watoto wanapata elimu na huduma zingine na kuhakikisha usalama wa nchi upo ndiyo kuheshimisha utu wa Mtanzania.

"Ndugu zangu, mengine niachieni mimi, matusi niachieni mimi, nayabeba kwa niaba yenu, manabii wetu Bwana Yesu alisulubiwa kwa kukomboa watu kwa ajili ya Mungu, lakini alikuwa anakomboa watu. Muhammad alipigwa mpaka akatolewa meno kwa kufanya kazi ya kukomboa watu kwa amri ya Mwenyezi Mungu.

"Samia Suluhu aliapa kuitumikia Tanzania na ndicho ninachokifanya, niliapa kulinda nchi na ndicho ninachokifanya, niliapa kujenga utu wa Mtanzania na kuheshimisha utu wa Mtanzania, ndicho ninachokifanya. Ninapohakikisha watu wanapata majisafi, watoto wetu wanapata elimu umeme upo, usalama wa nchi upo, ni kuheshimisha utu wa Mtanzania," alisema.

Alisisitiza kwamba hana uchungu kubeba matusi yote yanayotolewa kwa sababu anafanya kazi hiyo, hana uchungu hata kidogo wala hajutii, kwa hiyo amewaomba kura wananchi wa Ubungo na Kinondoni," amehitimisha mgombea huyo.

**Kauli za wagombea**

Kwa upande wake, mgombea ubunge wa Jimbo la Mkuranga, ambaye ni Waziri wa Ujenzi, Abdallah Ulega alisema Serikali ya Samia imetoa zaidi ya Sh1.7 trilioni katika miradi ya kupunguza msongamano na mafuriko jijini Dar es Salaam.

"Ulitupa maagizo mawili, kuondoa msongamano na kupunguza mafuriko. Fedha hizo zimetolewa na hii inaonyesha utu wako kwa kugusa maisha ya Watanzania," alisema Ulega.

Naye Mgombea ubunge wa Iramba Mashariki, Dk Mwigulu Nchemba alisema Serikali inayoongozwa na Samia imeleta mageuzi makubwa katika sekta ya biashara jijini Dar es Salaam kwa kuondoa kodi zisizo za haki zilizokuwa zikiwaelemea wafanyabiashara.

CamScanner